

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA THELATHINI NA SABA**

**26 MEI, 2021**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA SABA – TAREHE 26 MEI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu

ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

### III. MASWALI:

#### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

#### 305. MHESHIMIWA JONAS WILLIAM MBUNDA (MBINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

- Je, ni lini Serikali itaanza kujenga Barabara ya Kijiji cha Uzena kwenda Kijiji cha Njomlole katika Jimbo la Mbinga Mjini kwa kiwango cha changarawe ili iweze kupitika kwa wakati wote.

#### 306. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA (ULYANKULU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ipo tayari kutenga fedha kwa ajili ya kumaliza ujenzi wa Vituo vya Afya vya

Mwangozo na Uyowa katika Jimbo la Ulyankulu.

**307. MHESHIMIWA MOHAMED LUJUO MONNI (CHEMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Barabara ya Kwamtoro – Sanzawa mpaka Mpendo yenye km 58.2 itajengwa kwa kiwango cha kupitika msimu mzima kwani kwa sasa imekatika kutokana na mvua kubwa na kutojengwa kwa muda mrefu.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**308. MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN CHIVELESA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Nyamuirembe – Chato mpaka Katoke Biharamulo km 50 kwa kiwango cha lami.



**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**309. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA  
MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya,  
Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na  
Watoto:-

Je, ni lini Serikali itamaliza Ujenzi wa  
Hospitali ya Mkoa wa Katavi.

**WIZARA YA KILIMO:**

**310. MHESHIMIWA STELLA SIMONI FIYAO  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-  
Asilimia 70 ya Wakazi wa Mkoa wa Songwe  
wanategemea kilimo:-

Je, ni lini Serikali italetta pembejeo za kilimo  
kwa bei nafuu ambayo Wakulima wengi  
wataweza kumudu.

**WIZARA YA MAJI:**

**311. MHESHIMIWA BUPE NELSON  
MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Mradi mkubwa wa Maji wa Kabwe katika Wilaya ya Nkasi utakamilika.

**312. MHESHIMIWA BENAYA LIUKA KAPINGA (MBINGA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza upatikanaji wa maji katika Mji Mdogo wa Ruanda Wilayani Mbinga.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**313. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga Mahakama Hydrom katika Jimbo la Mbulu Vijijini.

**WIZARA YA NISHATI:**

**314. MHESHIMIWA ATUPELE FREDY MWAKIBETE (BUSOKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Maji kutoka Mto Rumakali katika Kata ya Lufilyo utaanza.

#### **WIZARA YA MADINI:**

#### **315. MHESHIMIWA GHATI ZEPHANIA CHOMETE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali ina Teknolojia gani mbadala ambayo itaepusha kutumia magogo kama matimba kwenye mashimo ya migodi hasa maeneo ya Nyamongo, Tarime, Buhemba na Butiama.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**DODOMA  
26 MEI, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**